

# HALMASHAURI YA WILAYA YA KITETO

SIMU NA: 027 - 2552000  
MOB NA: 0677 - 010213  
FAX NA: 027 - 2552020  
Email: [ded@kitetodc.go.tz](mailto:ded@kitetodc.go.tz)  
[info@kitetodc.go.tz](mailto:info@kitetodc.go.tz)  
Tovuti: [www.kitetodc.go.tz](http://www.kitetodc.go.tz)



OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI (W),  
S.L.P. 98,  
KIBAYA - KITETO

Kumb. Na. HMW/KT/V/21/VOL.II/107

Tarehe: 04 Novemba, 2020

## TANGAZO LA KAZI

**MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA KITETO ANAPENDA KUWATANGAZIA WANANCHI WOTE WENYE SIFA KUOMBA NAFASI YA KAZI IFUATAYO:**

**MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II (NAFASI 1)  
SIFA ZA MWOMBAJI:**

- Awe na Elimu ya Kidato cha Nne (Form IV)
- Awe amehitimu Mafunzo ya Astashahada/ Cheti cha Utunzaji wa Kumbukumbu katika mojawapo ya fani za Afya, Masjala, Mahakama na Ardhi.

**KAZI NA MAJUKUMU:**

- (i) Kutafuta kumbukumbu / nyaraka/ majalada yanayohitajika na wasomaji
- (ii) Kudhibiti upokeaji, uandikishaji wa kumbukumbu wa nyaraka.
- (iii) Kuchambua, kuorodhesha na kupanga kumbukumbu/ nyaraka katika makundi kulingana na somo husika (Classification and boxing) kwa ajili ya matumizi ya ofisi.
- (iv) Kuweka/ kupanga kumbukumbu / nyaraka katika reki, katika Masjala vyumba vya kuhifadhia kumbukumbu.
- (v) Kuweka kumbukumbu (barua, nyaraka) kwenye majalada.

**MSHAHARA:**

Ngazi ya Mshahara wa Serikali ni **TGS B** kwa mwezi.

**MAELEZO YA JUMLA NA UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI:**

1. Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45.
2. Waombaji wote waambatanishe na nakala za vyeti vya elimu, taaluma, cheti cha kuzaliwa na picha ndogo mbili za rangi (passport size).
3. Waombaji wote waaambatanishe na maelezo binafsi yaliyojitosheleza na yawe na anuani na namba ya simu.
4. Waombaji waliosoma nje ya nchi waambatanishe uthibitisho wa vyeti vyao kutoka Baraza na Mamlaka husika (TCU na NECTA).
5. Waombaji watakaoitwa kwenye usaili watatakiwa waje na vyeti halisi (Original Certificates).
6. Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

**Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto,  
S.L.P 98,  
KITETO.**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **16/11/2020** saa **9:30 Alasiri**.

Tamim H. Kambona  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
KITETO**

